Somo la 20

MAFUNZO YA BIBLIA KUHUSU IBILISI (Sehemu ya 3)

"Je, sikuwachagua ninyi kumi na wawili, na mmoja wenu ni ibilisi (diabolos)?" Yohana 6:70

"Vivo hivyo wake zao na wawe wastahivu; si wasingiziaji (diabolos)" 1 Timotheo 3:11

Tumeona kwamba 'shetani' ni neno la kawaida la Kiyahudi maana yake 'adui', na ni hivyo inavyotumika katika maandiko; Malaika na hata Mungu mwenyewe huwa 'mashetani' au wapinzani, kama mazingira yanavyohitaji. Neno 'ibilisi' hutumika kwa kubadilishana na shetani katika sehemu nyingi katika Biblia. Lakini inafaa Ikumbukwe kwamba neno 'ibilisi', wakati limetumika, kama 'shetani', kwa watu tofauti, kamwe haijatumiwa katika maana ifaayo, ambapo 'shetani' (adui) wakati mwingine ndiye anatajwa.

IBILISI - NOMINO YA KAWAIDA INAYOMAANISHA MSHITAKI AU MCHONGEZI

Neno 'Ibilisi' ni tafsiri ya (na limetokana na) neno la Kigiriki 'diabolos' nomino ya kawaida maana yake 'mshitaki, mchongezi'. Ni mchanganyiko wa dia, 'kwa njia ya', na ballo, 'kupiga'. Kwa hivyo inamaanisha 'kushambulia kwa njia ya'. Kwa njia ya mfano ina maana 'kumchoma kwa mashtaka au kutoa ripoti mbaya'. Maandishi ya Parkhurst imefafanua diabolos kama 'mshitaki, mchongezi. Kitabu cha Strong kinatoa 'tafsiri,' yenye maana ya 'mshitaki'.

Tunaona kwamba diabolos, kama vile Shetani, ni nomino ya kawaida, na sio jina sahihi. Kama vile Yesu alivyotumia 'shetani' kwa Petero, hivyo alitumia Ibilisi kwa Yuda (tazama Yohana 6:70 hapo juu). Yuda alikuwa mwongo, msaliti na mshitaki. Kwa hivyo alikuwa 'ibilisi'. Paulo alitumia hasa neno hilo moja (diabolos kwa Kigiriki) kuelezea wanaume na wanawake ambao hawengeongozwa na tabia za utauwa. "Vivyo hivyo wake zao na wawe wastahivu; si wasingiziaji (diabolos)" - 1 Timotheo 3:11.

"Watu watakuwa .. wasiowapenda wa kwao, wasingiziaji (diaboloi)" - 2 Timotheo 3: 2-3.

"Vivyo hivyo na wazee wa kike…, hali kadhalika .. wawe na mwenendo wa utakatifu; si wasingiziaji (diabolous) – Tito 2:3

Neno 'ibilisi' katika maeneo haya matatu haionekani katika matoleo ya kawaida ya Biblia, lakini imetafsiriwa vizuri' kwa namna ya kufikisha maana sahihi. Lakini Watafsiri hawajakuwa waaminifu katika maeneo mengine, na kwa hivyo wamesababisha mkanganyiko. Kama wangetafsiri neno la Kigiriki 'diabolos' mara kwa mara, na kuwa Biblia ingejitafsiria, kama inavyotakiwa, na kama ilivyo …wakati inasomwa na kuchunguzwa katika mfumo wa lugha yake asili,

ISHARA ZA KISIASA. PEMBE KUMI NI SAWA NA WAFALME KUMI

Hii ni wazi kwa yale Kristo aliwaambia wafuasi wake waaminifu kuhusu mamlaka ya kipagani ya Kirumi kuwatesa na kuwanyanyasa -"Ibilisi (diabolos) atawatupa baadhi yenu gerezani" (Ufunuo 2:10). Ni hakika mamlaka ya kisiasa ambayo huwaweka wafuasi hao gerezani. Tunajua jinsi serikali ya Kirumi iliwatesa Wakristo wa awali. Haya ni mamlaka ya nguvu duniani, yaliyopangwa kisiasa kama Pagani au mamlaka ya Papa, kama yalivyo katika kitabu kwa sura - "Joka, yule nyoka wa zamani, ibilisi (diabolos) na shetani" (Ufunuo 20: 2). Hili lilikuwa ni 'Joka' lililokuwa na Pembe kumi, ambalo linaelezwa kuwa 'wafalme kumi'(Ufunuo 17:12): ni wazi hii ni ishara ya kisiasa. Hizi ni tawala za kisiasa na dini za ulimwengu wa dhambi, zinazoundwa kutokana na mkusanyiko wa wanaume na wanawake wanaotenda dhambi. Kwa ujumla, ni wachongezi kwa Mungu na waangamizaji wa wanadamu.

KWA UJUMLA, 'IBILISI' NI KANUNI YA DHAMBI KATIKA WANADAMU WOTE

Katika matumizi yake ya ujumla, neno 'ibilisi' (diabolos) inatumika kwa kanuni ya dhambi iliyopo katika kila mtu binafsi wa uzao ya Adamu, kama mizizi ya Ibilisi yote iliyopangwa na kudhihirishwa. Huu ni mfano katika matumizi yake kwa Kristo katika Waebrania 2:14

"Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye (Yesu) naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi."

IBILISI MAARUFU, makisio ya jadi ni kwamba Ibilisi ni jitu - kuu, linalodumu, kivitendo ni hayawani mwenye nguvu zote, mwenye uwezo wa kuwajaribu na kuwanyanyasa mamilioni duniani, na wakati huo huo akishughulikia adhabu wanayopata mabilioni kuzimuni, matokeo yake yangedhihirisha mambo manne ya kiumbavu –

1. Kwamba Mwana wa Mungu alikuwa achukue udhaifu wa mwili wa binadamu ili aweze kumharibu ibilisi. Paulo hapa anasisitiza umuhimu huu, na anaeleza wazi wazi kuwa yeye kwa kweli hakuchukua maumbile ya nguvu ya malaika (kifungu cha 16).

2. Fikiria jitu lenye nguvu , zaidi ya binadamu, mwenye uwezo wote, aharibiwe na kiumbe dhaifu kwa kifo chake!

3. Kwamba kwa njia kama ilivyotajwa hapo juu, Kristo 'kwa kifo chake alimharibu ibilisi,' ibilisi lazima sasa awe amekufa, kaharibiwa. Lakini inavyoonekana kwa sasa, ibilisi ameata nguvu zaidi sasa kuliko hapo awali, kwa hakika, 'dini za jadi' zingekosa cha kuhubiri bila kuwa na ibilisi huyu wao. Ukweli ni kuwa, 'Ibilisi' wa Biblia aliharibiwa katika kifo cha Kristo, na - kama inavyomhusisha Kristo mwenyewe - sasa huyu ibilisi amekufa na kuharibiwa kabisa. "Ibilisi" wa kweli wa Biblia sio kitu zaidi ya 'mwili ulio na dhambi' (Warumi 8: 3) na 'sheria ya dhambi' (Warumi 7:23) na, kwa hivyo, imeharibiwa milele katika Kristo (huo ulikuwa ushindi wake), na hatimaye pia wale wote ambao ni sehemu ya mwili wake watamwangamiza huyu ibilisi.

4. Kwamba ibilisi, kama jitu , ana 'nguvu za mauti'. Kwa upande mwingine, Biblia inatangaza kwamba kanuni za dhambi katika wanadamu – inayohaiishwa kama 'ibilisi' – ana nguvu za mauti. Hii ina mantiki, ni nafuu. Maandiko yanatwambia kwamba kabla ya Yesu kuvunja milango yake ya gereza, ilikuwa imemfunga mwana wa Adamu katika minyororo ya chuma yake isiyoepukika. 'Mshahara wa dhambi ni mauti', na wote bila ubaguzi walitenda dhambi. Lakini kuwazia hayawani au jitu lisilopatikana na mauti – adui mkuu wa Mungu na mwanadamu - kuwa ana nguvu za mauti ni wazo la kutisha na haliwezekani. Ni Mungu, na ni Mungu peke yake, aliye na nguvu za mauti. Hakika 'nguvu za mauti' ni za mwisho na zenye uwezo mkuu, na hayo ndiyo mtu anaelewa. Au tunafaa kuamini huyu hayawani, ambaye huwatesa mabilioni milele kwa kujifurahisha, ni wakala wa Mungu, na kwamba Mungu amempa mamlaka ya kifo juu ya wanadamu? Kweli hii inaafikiana na miungu ya Kigiriki na Kirumi na ushirikina ambapo tunapata hii picha, lakini si Mungu mtakatifu wa maandiko na wa Kweli. Anasema:

"Naua Mimi, na mimi nahuisha" (Kumbukumbu la Torati 32:39).

KUSUDI LA KIFO CHA KRISTO ILIKUWA KUHARIBU DHAMBI

Vile vile maneno ya Paulo katika Waebrania 2, Yohana anasema kwamba Yesu –

"Alidhihirishwa ili azivunje kazi za Ibilisi" (Yohana 3: 8).

Ibilisi ambaye Kristo alikuja kuharibu ni Dhambi –

"Alikuja kuziondoa dhambi zetu" (Yohana 3: 5).

"Azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake" (Waebrania 9:26).

"Tazama Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu" (Yohana 1:29).

"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti" (1 Petro 2:24).

Hii nukuu ya mwisho ni muhimu hasa. Ilifanyika 'KATIKA mwili wake mwenyewe', chochote kilichokuwa kimefanikishwa katika maisha yake na kifo. Hii ina mahusiano ya karibu na umuhimu wa yeye kuwa “mwili na damu” na ya ‘mwili ulio na dhambi' kwa lengo la kuharibu ibilisi katika kifo chake.

Kristo, kwa njia ya kifo, aliharibu 'dhambi ya ulimwengu' - 'ibilisi' wa Biblia (Waebrania 2:14). Katika mwili wake. kama mwakilishi (mtu mwenye mwili huo wa dhambi kama binadamu wengine), mtu kujitolea kuchukua jamii yote, akaharibu nguvu ya dhambi kwa:

1. Kuwasilisha kikamilifu mapenzi ya Mungu katika maisha yake yote (kupinga kabisa na kushinda tabia ya kutenda dhambi);

2. Kupigilia mwili wa kufa kwenye 'mti' (msalaba);

3. Kuepuka mauti kwa kufufuka kutokana na haki yake kamilifu katika njia zake zote;

4. Kuishi milele, tangu hapo milele pasipo na ibilisi (diabolos) dhambi mwenendo wa dhambi na nguvu za mauti.

Ushindi huu dhidi ya nguvu ya dhambi ('ibilisi') Kibiblia inaelezwa kama –

"Mungu kwa kumtuma mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili" (Warumi 8: 3).

NI DHAMBI AMBAYO INA NGUVU ZA MAUTI

"Dhambi katika mwili 'ni ‘ibilisi’ ambayo iliharibiwa na Yesu katika kifo chake. Huyu ni ibilisi aliye na mamlaka juu ya kifo; kwa kuwa ni dhambi, na hakuna kitu kingine ila dhambi, ambayo husababisha mauti kwa wanadamu. Hivyo tunasoma - "Kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti" (Warumi 5:12). "Mauti ililetwa na mtu" (1 Wakorintho 15:21). "Mshahara wa dhambi ni mauti" (Warumi 6:23). "Dhambi ilivyotawala katika mauti" (Warumi 5:21). "Dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti" (Yakobo 1:15). "Uchungu wa mauti ni dhambi" (1 Wakorintho 15:56).

Bila shaka, kihalisia, ni Mungu aliye na 'mamlaka juu ya kifo’, maana yeye ana uwezo wote. Hakuna mtu mwingine (kwa hakika hatuzungumzii Yule muovu) anaweza kumiliki au kudhibiti yale madaraka. Lakini kwa vile dhambi ilileta kifo hapo mwanzo, na dhambi bila kuepukika (katika mwenendo wa kawaida) huzaa kifo, na dhambi ni yenye mauti hivyo, kanuni ambayo haiepukiki (katika mwenendo wa kawaida) inamfanya Mungu mtakatifu kuleta kifo - ni jambo sahihi tena kamilifu na inaeleweka kusema kuwa dhambi 'ina nguvu za mauti

'SHERIA yA DHAMBI VIUNGONI MWANGU'

Lakini ni nani au nini huwashauri wanaume na wanawake kutenda dhambi dhidi ya Mungu? Ni nini husababisha dhambi? Yakobo anajibu hili kwa uzuri na uwazi sana - "Kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti. " (Yakobo 1: 14-15) Paulo anataja hii kama: "SHERIA KATIKA VIUNGO VYANGU, ikipigana na sheria ya akili zangu" (Warumi 7.23). Dunia nzima hutii au kutumikia sheria hii, na kwa hiyo “hukaa katika yule mwovu"(1 Yohana 5:19). Yohana hivyo anaeleza hali hii ya duniani - "KILA kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia" (1 Yohana 2:16). Sheria hii inaweza kuondolewa tu kupitia kwa nguvu za Neno la Mungu. Hivyo Yesu alisema - "maneno niliyowaambia, ni Roho, ni uzima" (Kuleta mwangaza wa Ukweli wa Mungu, ikija kutoka nje, inatanguliza sheria mpya katika akili: takatifu, sheria ya kuleta uzima wa Roho wa Mungu. Hii inajenga migogoro ya ndani: "sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili, kwa maana hizi ZIMEPINGANA" (Wagalatia 5:17).

Mafanikio ya vita dhidi ya sheria hii ya mwili, au kanuni imara ya uasi, katika maisha yote ya Kristo, ni jinsi alivyoshinda 'dhambi katika mwili', au 'ibilisi' (diabolos). Kwa hivyo pia ni lazima daima kujitahidi kushinda sheria hii ya dhambi katika viungo vyetu. Hivyo mara kwa mara tunaonywa na kuamriwa - "Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake" (Warumi 6:12).

"Enendeni kwa Roho, nanyi hamtazitamani tena tamaa za mwili" (Wagalatia 5:16).

"Kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki." (Warumi 6:16).

"Kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; bali Kama mkiyafisha (kuua) matendo ya mwili, kwa Roho, mtaishi" (Warumi 8:13).

Hakuna ibilisi jitu, aliye na pumzi ya moto na pembe na kwato. Lakini kuna ibilisi, ibilisi wa BIBLIA. Ibilisi ni hali ya mwanadamu mwenyewe katika mwelekeo uliokita mizizi ya kimwili -, 'sheria ya dhambi katika viungo vyake "ambayo huvutwa kuelekea kuasi amri takatifu, za haki na busara ya Mungu -" Atendaye dhambi ni wa Ibilisi "(1 Yohana 3: 8).

TASHHISI NI TAMATHALI YA USEMI WA KAWAIDA WA MiFANO YA KIBIBLIA

Kusiwe na ugumu na dhana ya 'ibilisi' wa Biblia kuhaiishwa. Mambo mengi na mawazo yamepewa uhai kwa ufanisi katika Maandiko.

Hekima: "Hekima .. yeye ana thamani kuliko fedha. . Ana wingi wa siku katika mkono wake wa kulia, na kwa mkono wake wa kushoto ana mali na heshima "(Mithali 3: 13-15).

Utajiri:" huwezi kutumikia mabwana wawili: Mungu na mali "(Mathayo 6:24)

Tabia zetu : "Kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake" (Wakolosai 3: 9). "Mvue utu wa zamani... mfanywe wapya" (Waefeso 4:22-24) "Utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye "(Warumi 6: 6).

Hali: Miti, jua, mafuriko, vilima, maeneo ya taka, nk yamesawiriwa yakiimba, kupiga makofi, kuwa na furaha, kucheza, kuruka, na kufanya mambo mengine ya kibinadamu.

Kuongezea. Na, juu ya yote, Dhambi yenyewe – Ibilisi wa Biblia - ni hivyo anahaiishwa - "DHAMBI ilivyotawala katika mauti" (Warumi 5: 21). "DHAMBI ikafanya ndani yangu .. DHAMBI ikaniua mimi .. DHAMBI alinidanganya" (Warumi 7: 8-11). "Ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake kwa kumtii, mmekuwa watumwa wake, kwamba ni utumishi wa DHAMBI.." (Warumi 6:16). "Kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi" (Yohana 8:34). "DHAMBI isitawale ndani ya miili yenu hata mkazitii tamaa zake '(Warumi 6:12).

Kutokana na hili, tunapaswa kutarajia' diabolos ', ‘maumbile ya dhambi', ‘sheria ya dhambi katika viungo, 'kuhaiishwa’, la sivyo ingeshangaza.

NYOKA-CHANZO CHA DHAMBI

Dhambi ni mchongezi mkubwa ya Mungu, katika kukanusha ukuu wake, hekima, wema, na Ukweli wa Neno lake. Kwa hivyo Dhambi inaitwa . 'mshitaki, mtukanaji, mwongo, na mawazo haya yanaitwa ibilisi katika neno la Biblia, na inaeleweka vema

Maelezo ya Biblia juu ya chanzo cha Dhambi yanaonyesha istilahi hizi zimefaa kutumika. Kosa la awali la Adamu halikutoka ndani mwake. Ilishauriwa na Hawa; na ya Hawa ilishauriwa na nyoka; "Nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu." (Mwanzo 3: 1)

Nyoka, alipewa na Mungu kwa muda uwezo wa kusema, alidokeza hoja ya uongo kuhusu mti wa ujuzi wa mema na mabaya; yaani, kwamba kwa kula kutoka kwake Adamu na Hawa hawatakufa bali wataishi milele, kwa sababu (yeye alidhania) wangeweza kuwa 'kama malaika; na Malaika huishi milele. Kwa hivyo Nyoka akamwambia, ‘Nyinyi Hakika hamtakufa.’ Ni kweli kuwa kula kwa mti uliwafanya kuwa kama Malaika katika mambo fulani (Mwanzo 3:22).

Kwa hivyo nyoka alikuwa mchongezi na mwongo katika kutangaza kauli ya Mungu. 'Nyinyi hakika mtakufa’ kuwa haikuwa kweli. Kwa hivyo Nyoka akawa ishara na 'baba' ya yote yanayotokana na uwongo huo: kanuni iliyojengeka ya uasi, na dhambi zote zilizofuatia.

Kutokana na nyoka kusababisha mtu kuanguka, Mungu alisema (Mwanzo 3:15) hivyo itafanya uadui kati ya uzao wa nyoka (watu waovu, waongo na wasio watiifu) na mbegu ya mwanamke (watu wema, walio jikita katika Kristo) mpaka wakati ambapo uzao wa mwanamke hatimaye utaharibu uzao wa nyoka. Embe huzaa embe. Hii ndiyo sababu dunia nzima ya maumbile ya binadamu iyanazungumziwa kama nyoka na ibilisi.

Dhana ya uasi imepandwa katika akili ya wazazi wetu wa kwanza na ni kupitia kwa nyoka, na ambayo ilikuwa sheria ya asili yao (Warumi 7:23), imeletea dunia ya wanaume na wanawake ambao awali, iliyo na mtazamo wa kimwili na kutomtii Mungu. Hivyo wao ni wa asili na tabia ya asili 'kizazi cha nyoka' (Mathayo 23:33), kama Kristo alivyosema: "Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi (mchongezi), na tamaa za baba yenu mtafanya" (John 8:44).

WOTE KWA ASILI NI WA WATOTO WA ‘IBILISI’

Wote ambao ni wazao wa Adamu kwa asili ni ‘watoto wa ibilisi’. Mwili wao wa kufa unaeleza haya, kwa sababu kifo ni matunda ya nyoka (ibilisi, mchongezi) aliyedanganya, na kusababisha Adamu kutotii. Lakini wote waliohusiana na 'Adamu wa pili' (Kristo) wanaachiliwa na familia ya 'ibilisi' (dhambi), na kuwa wana wa Mungu.

Uharibifu wa 'ibilisi' na kazi ya Kristo ni ushindi na ya mwisho ya kuondolewa kwa asili dhambi ya binadamu. Hii inakamilishwa kwanza katika Kristo mwenyewe - kama mfano - na utiifu kamili kwa Baba yake, na kwa kutii kwa kifo cha mtini: mtiifu, kwa hiari, kusulubiwa kwa umma na kuasi asili ya laana ya dhambi katika kutoa haki za sheria ya Mungu na kuonyesha utakatifu wa Mungu; na kwa ufufuo wake aishi maisha ya milele; na hivyo –

"Wala mauti haimtawali TENA." (Warumi 6: 9)

MCHAKATO WA VIZAZI VYA MUDA KATIKA UHARIBIFU WA 'IBILISI'

Baada ya hapo, mchakato wa uharibifu wa ibilisi bado inaendelea katika karne zote, kama wale ambao wamekuwana uhusiano na sadaka ya Kristo kwa njia maalumu ya imani, ubatizo na maisha ya utiifu kuyashinda maisha yao ya kutenda dhambi kwa nguvu za Neno la Mungu zinazoendeshwa kwa mawazo yao na katika maisha yao. Kwa wote ambao wamefanya hivi, kwa nguvu zao zote, waliojitahidi kumpendeza Mungu, watapewa uzima usio na mwisho mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo atakaporudi duniani. Watakuwa wamekuwa waaminifu na kufanikiwa (ingawa sio kwa ukamilifu) wamefanya kazi ya kuangamiza au 'kuweka chini' (1 Wakorintho 9:27) msukumo wa kutenda dhambi ('ibilisi' ndani yao) katika maisha yao yote. Kubadilishwa kwao na kupata miili ya kuishi milele na 'asili ya Mungu' (2 Petero 1: 4) itakuwa uharibifu wa mwisho wa ibilisi, kama ilivyokuwa kwa Kristo karne nyingi zilizopita.

Waovu wanaowajibika, wa sasa na wa siku za majira ya nyuma (wafu kufufuliwa, walio hai wakusanywe) pia atakaporudi Kristo watahukumiwa, na kisha kuadhibiwa kwa kipimo, kwa mujibu wa matendo yao (Luka 12:47), na hatimaye kuondoa milele hii hali ya asili ya ibilisi kutoka duniani.

Kisha, wakati wa miaka 1000 ya utawala wa Kristo duniani, mataifa yatafundishwa kuwa wenye haki, na watamjua Mungu (Yeremia 31:34), na wataitwa - kupitia kwa imani na upendo wa Mungu – ili kushinda msukumo wa miili yao ya kibinadamu, na kuishi katika utakatifu. Mwisho wa miaka 1000 kutakuwa na hukumu nyingine ya wote ambao wameishi katika miaka 1,000. Wote ambao wamefariki katika kipindi hicho watafufuliwa, na wote – walio hai na wafu - watahukumiwa. Wale ambao wamekuwa watiifu watapewa uzima wa milele (kama wale wa kipindi hiki cha sasa watakavyokuwa katika kurudi kwa Kristo), na wale ambao hawakuwa watiifu wataangamizwa.

Hivyo, wote walioachwa hai watakuwa wenye uzima wa milele. Dhambi na mauti vitakuwa vimeondolewa kutoka duniani. Kutenda dhambi kwa sasa, kufa, asili ya kufa kwa wanadamu - iliyoletwa juu ya dunia na dhambi ya Adamu - itakuwa imekwenda milele. Hivyo 'Ibilisi' atakuwa ameharibiwa kabisa, katika kila kipengele na udhihirisho. Kazi kubwa ya Kristo itakuwa sasa imekamilika kwa ushindi, na atawachia mambo yote yawe kwa mkono wa Mungu, kwamba Mungu mwenyewe aweze sasa kuwa ‘YOTE KATIKA WOTE’ (1 Wakorintho 15: 24-28).

MAJARIBU YA KRISTO – ‘KAKANDAMIZWA NA IBILISI'

Inabainika kuwa idadi yenye haki ya kuonekana ya neno ibilisi kutokea katika rekodi za majaribu ya Kristo jangwani, mara tu baada ya ubatizo wake na kushukiwa na Roho juu yake. Wazo la othodoksi kwamba alikuwa ‘anaongozwa na Roho' (Mathayo 4: 1) ili ajaribiwe na Ibilisi wa Othodoksi, adui mkuu wa Mungu, ni kushusha hadhi ya tahadhari ya taswira nzima ya Mungu, kama vita katika mbingu takatifu kwa Mungu kati ya malaika waaminifu na waasi.

Kuwa hivyo itakuwa majaribu yoyote halisi ya Kristo - na ufahamu wake, na alivyo karibu na, Mungu - kupata pendekezo kutoka kwa adui wa Mungu ni vigumu kuamini. Ni ya kuwazia kivingine. Inafaa yawe ni majaribu ya kuaminika, kama ilivyo tabia na ufahamu wa Kristo. Ni nani ambaye alitoa nyanja ya nje ya majaribu hatuambiwi. Mamlaka ya Kirumi yamependekezwa na pana uwezekano mkubwa, wao kujaza mahitaji hayo. Hakika wao ndio walioweza hasa kujaza nafasi halisi ya kisiasa ya ibilisi.

'Walioonewa na Ibilisi’ (Matendo 10:38) inatumika kwa jumla ya magonjwa yote, kwa sababu Dhambi, na laana na maovu yaliyokuja kwa wanadamu kupitia kwa Dhambi (Mwanzo 3: 17-19) ni chanzo cha ulemavu wote na magonjwa.

MAPEPO: MAGONJWA NA MATESO

Neno 'ibilisi' hutokea mara nyingi zaidi katika KJV Agano Jipya (kawaida kwa wingi), lakini neno la awali katika mifano hiyo sio 'ibilisi', lakini 'mapepo', na hutumika katika kurejelea magonjwa, kimwili na kiakili. Hii ni hasa kutokana na upekee wa lugha ya Kigiriki, na ya dhana iliyo tayari katika asili ya hotuba ya kipindi hicho.

Ilikuwa ni desturi katika nyakati za Biblia - wakati mgonjwa alizungumza au kutenda chini ya ushawishi wa maradhi - kuitaja kama 'mapepo' kuzungumza au kutenda; kama vile tunaposema 'kinywaji kinazungumza' wakati tunataka kuonyesha kwamba kauli ya mtu mlevi ni matokeo ya ulevi na si wa mawazo ya busara. Wale ambao walitumia aina hii ya kauli kutambua kwamba maneno na matendo yalikuwa hasa yale ya mgonjwa mwenyewe, lakini walikuwa wanaonyesha kwamba kusema au kutenda huko ilikuwa inasababishwa na ugonjwa. Magonjwa yalijulikana kama ‘mapepo’ au ‘daimon’kwa sababu maneno yalitokana na imani ya ushirikina katika viumbe viitwavyo ‘mapepo’ yanayosababisha magonjwa. Lakini yeyote anayetumia maneno ya kawaida bila shaka hatakuwa anamaanisha asili yake. Tukiweza kufuatilia asili ya mwenyeji wa maneno ya Kiingereza au Kiswahili kwa asili ya ajabu na ushirikina, lakini tunazitumia bila mawazo yoyote beni - au hata ufahamu wa -- asili hizo.

Inabainishwa kuwa hakuna maneno kama hayo katika kujadili ugonjwa wote kupitia Agano la Kale, ambayo yako katika Kiyahudi. Katika lugha ya Kiingereza au Kiswahili tuna maneno kama hayo yanayoelezea magonjwa fulani ambayo tunatumia kwa uhuru bila kufahamu hata kidogo asili yao halisi au maoni, kama 'kichaa' (kutokana na kupatwa na mwezi), ‘Densi’ ya

‘Mtakatifu Vitus’ (inayoweza kutibiwa na ibada ya Mlinzi mtakatifu wake), na mengineo kama mateso ya kimwili kama ‘Mtego wa Ibilisi’, nk.